
# TCCIA INVESTMENT PLC

MKUTANO MKUU WA MWAKA
WA 15 WA WANAHISA 22/08/2020



# TAARIFA YA KAMPUNI

## Kwenye Mkutano Mkuu wa 15 wa Wanahisa

**Dondoo Na. 15/1/2020**

## TAARIFA YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TANO UTAKAOFANYIKA SIKU YA JUMAMOSI TAREHE 22 AGOSTI 2019.

Tunapenda kukujulisha kuwa Mkutano Mkuu wa Kumi na tano wa Wanahisa wa TCCIA Investment PLC, utafanyika siku ya Jumamosi tarehe 22 Agosti, kwa njia ya mtandao. Mkutano utaanza saa Tatu kamili (3.00) asubuhi. Kampuni itawatumia Wanahisa wote kupitia simu zao za mkononi utambulisho na maelekezo kuhusu jinsi ya kujiunga na kushiriki Mkutano Mkuu kidijitali.

Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano ni:

1. Kufungua Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano;
2. Kupokea na kuthibitisha mabadiliko kwenye Kanuni za Kampuni;
3. Kupokea na kuridhia Dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano;
4. Kuthibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne;
5. Kupokea, kujadili na kuridhia utekelezaji wa Maazimio ya Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne;
6. Kupokea, kujadili na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi wa Bodi ya Kampuni na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2019;
7. Kupokea na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Gawio kwa Mwaka 2019;
8. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu uteuzi wa Mkaguzi wa Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia 31 Desemba, 2020;
9. Kupokea, kujadili na kuridhia pendekezo la Bodi kuhusu Malipo ya Wajumbe wa Bodi 10. Kupokea, kujadili na kuamua mapendekezo kutoka kwa Wanahisa;
11. Kufunga Mkutano Mkuu wa Kumi na Tano.

**MAELEZO:**

1. Mapendekezo yote kutoka kwa wanahisa yatakayojadiliwa katika dondoo namba 10 yatumwe na kumfikia Katibu kabla tarehe 10 Agosti, 2020.
2. Taarifa ya Mwaka 2019 na Makabrasha ya Mkutano yatapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https://www.tcciainvest.co.tz) na kuanzia tarehe 10 Agosti, 2020.
3. Endapo Mwanahisa atashindwa kuhudhuria anaombwa kuteua Mwakilishi atakayehudhuria mkutano kwa niaba yake. Fomu ya Uwakilishi inapatikana kwenye tovuti ya Kampuni (https:// www.tcciainvest.co.tz). Fomu za Uwakilishi zilizojazwa zitumwe kwa Katibu kupitia barua pepe pkifunguomali@tcciainvest.co.tz au picha ya fomu ya uwakilishi iliyojazwa itumwe kwenye WhatsApp na 0757-138048 na kumfikia Katibu kabla ya tarehe 19 Agosti,2020.

Imetolewa kwa niaba ya Bodi ya Wakurugenzi.

........................................

**Peter W. Kifunguomali**

Katibu

**Bodi ya Wakurugenzi**

## MABADILIKO KWENYE KANUNI ZA KAMPUNI

Kutokana na hali ya sasa hasa ukizingatiwa kuibuka kwa magonjwa ya mlipuko na ukuwaji wa tehama ni wakati muafaka kwa kampuni kufanya Mikutano yake Mikuu ya Wanahisa kukutana ana kwa ana au kwa njia ya mtandao.

Bodi inapendekeza kifungu cha 86 kifanyiwe marekebisho kuwa Mkutano mkuu uhudhuriwe na wanahisa wasiopungua 10 wenye hisa zaidi ya asilimia 50 kutoka ishirini wa sasa. Kwa sasa mkutano mkuu unatakiwa kuhudhuriwa na wanahisa 50 wenye asilimia 20.

### UWASILISHAJI

Wanahisa wanaombwa kuongeza katika kifungu cha 47 na 86 cha Kanuni za Kampuni ili kuonyesha kuwa Mikutano Mikuu inaweza kufanyika kwa njia ya kukutana au kwa njia ya mtandao na idadi ya wanahisa kuwa 10 wenye hisa zaidi ya asilimia 50.

## "Azimio la 1/2020

**Imeazimiwa kwamba kifungu cha 47 kisomeke kuwa "Kampuni itafanya Mkutano Mkuu wa kila mwaka ama kwa Wanahisa kukutana ana kwa ana au kwa njia ya mtandao. Pia imeazimiwa kufanya marekebisho kwenye kifungu cha 86 kuwa Mkutano mkuu utahudhuriwa na Wanahisa wasiopungua 10 wenye hisa zaidi ya asilimia 50."**

**Dondoo Na. 15/3/2020**

# KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA WANAHISA ULIOFANYIKA SIKU YA IJUMAA TAREHE 10 AGOSTI, 2019 KATIKA UKUMBI WA MAKUMBUSHO YA TAIFA – DAR ES SALAAM.

## 14.1 WALIOHUDHURIA

**MWENYEKITI**

Bw. Fortunatus Magambo - Mwenyekiti

**KATIBU**

Bw. Donald J. Kamori - Katibu

### WANAHISA

Orodha ya Wajumbe pamoja na Wawakilishi wa Wanahisa waliohudhuria Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne uliofanyika siku ya Ijumaa tarehe 10 Agosti, 2019 imeambatanishwa kwenye Kumbukumbu hizi. Tafadhali angalia Kiambatisho Namba 1.

## 14.1 KUFUNGUA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE

Mwenyekiti alifungua mkutano kwa kuwakaribisha Wanahisa, Wajumbe wa Bodi, Wageni Waalikwa na Wafanyakazi wa Kampuni kwenye Mkutano mkuu wa 14 wa Mwaka. Baada ya Kutolewa taarifa kwamba Akidi ilikuwa imetimia kulingana na kifungu Namba 38 cha Kanuni za Kampuni, Mwenyekiti alifungua Mkutano saa 4:21 Asubuhi.

## 14.2 KUPOKEA NA KURIDHIA DONDOO ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE WA MWAKA

Hakukuwa na Mabadiliko yoyote hivyo Wajumbe walipitisha dondoo za Mkutano Mkuu wa Kumi na Nne kama zilivyosomwa na Katibu wa Bodi.

## 14.3 KUTHIBITISHA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TATU

Wajumbe walithibitisha Kumbukumbu za Mkutano Mkuu wa Kumi na Tatu na zikasainiwa na Mwenyekiti na Katibu.

## 14.4 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA MKUTANO MKUU WA KUMI NA TATU ULIOFANYIKA TAREHE 10 AGOSTI, 2018.

Taarifa ilitolewa kuhusu utekelezaji wa maazimio mbalimbali yaliyopitishwa na Wajumbe wakati wa Mkutano Mkuu wa Kumi na tatu uliofanyika tarehe 30 Novemba, 2018. Mambo muhimu ambayo yalitolewa taarifa ni:

### 14.4.1 AZIMIO KUHUSU MALIPO YA GAWIO

Taarifa ilitolewa kuwa Azimio hili limetekelezwa kwa kuwalipa Wanahisa ambao taarifa zao katika Daftari la Wanahisa zilikuwa zimerekebishwa. Kila Mwanahisa alilipwa shilingi 2.54 kwa kila hisa moja.

**14.7 KUPOKEA NA KURIDHIA PENDEKEZO LA BODI KUHUSU MALIPO YA GAWIO KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019.**

14.7.1 Kwa mwaka 2018, Bodi ilipendekeza kulipa Shilingi 2.54 kwa hisa moja ambayo ni sawa na Shilingi milioni 185. Pendekezo hili lilikubaliwa na wajumbe wa Mkutano Mkuu ambapo gawio lilianza kutolewa siku 90 baada ya kufanyika kwa Mkutano Mkuu wa 14 kama ilivyoamuliwa. Iliazimiwa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi kwamba, gawio la shilingi za Kitanzania 2.54/= kwa kila hisa, ambayo ni jumla ya shilingi milioni 185 kwa ajili ya kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2018 na lilipwe ndani ya siku tisini.

**14.8 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA PENDEKEZO LA BODI KUHUSU UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA 31 DESEMBA, 2018 PAMOJA NA MALIPO YAKE.**

14.8.1 Wanahisa waliombwa kupitisha uteuzi wa Kampuni ya CROWE Tanzania kuwa wakaguzi wa nje wa Kampuni kwa mwaka 2019 kwa ada ya shilingi za Kitanzania 17,525,000 kabla ya kodi. Iliazimiwa kwamba CROWE Tanzania wateuliwe kukagua mahesabu ya kampuni kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 31 Desemba mwaka 2019 kwa ada ya shilingi 17,525,000.

**14.9 KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA PENDEKEZO LA BODI KUHUSU MALIPO YA WAJUMBE WA BODI (DIRECTOR'S FEES).**

14.9.1 Mkutano Mkuu ulielezwa kwamba kwa mwaka 2018 Wajumbe wanaombwa kupokea, kujadili na kuidhinisha malipo ya Wakurugenzi kiasi cha Shilingi 4,000,000/= kwa kila Mkurugenzi. Pia Wajumbe walielezwa kuwa kiasi kinachopendekezwa na Bodi ni sawa na kilicholipwa mwaka 2017. Wanahisa waliazimia kwamba kama ilivyopendekezwa malipo yawe kiasi cha shilingi 4,000,000/=.

**14.10 KUPOKEA, KUJADILI NA KUAMUA KUHUSU DONDOO MBALIMBALI ZITAKAZOKUWA ZIMEWASILISHWA NA WANAHISA KABLA YA TAREHE 27 JULAI, 2019.**

14.10.1 Afisa Mtendaji Mkuu Ndugu Kamori alitoa taarifa kwamba atapenda kupumzika ifikapo Desemba 31, 2019 baada ya kuitumikia Kampuni kwa kipindi cha miaka 15 tangu Kampuni ilipoanza shughuli zake rasmi Januari 2005. Wajumbe waliazimia kwa kuiagiza Bodi kuangalia namna ya kumpongeza Afisa Mtendaji wa Kampuni, Ndugu Donald J. Kamori na Mhasibu wa Kampuni, Ndugu, Edgar L. Kahabwa wanaomaliza muda wao katika kuitumikia Kampuni.

**14.11 KUFUNGA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE.**

14.11.1 Mwenyekiti aliwashukuru Wajumbe wa Mkutano Mkuu kwa Majadiliano ya kina ambayo lengo lake ni kuimarisha shughuli za Kampuni. Aliwahakikishia wajumbe kwamba bodi itachukua hatua kutekeleza mambo yote yaliyoamuliwa na Mkutano Mkuu. Mwisho aliwashukuru Wanahisa kwa kuhudhuria na kufunga Mkutano saa 12.20 Mchana.

Katibu:.............................. Mwenyekiti.............................. Tarehe:..............................

Dondoo Na. 15/4/2020

## KUTHIBITISHA MUHTASARI WA MKUTANO MKUU WA KUMI NA NNE WA MWAKA ULIOFANYIKA TAREHE 10 AGOSTI 2019

### WASILISHO

Wanahisa wanaombwa kupokea na kuthibitisha Muhtasari wa Mkutano Mkuu wa Mwaka uliofanyika tarehe 10 Agosti 2019 kama kumbukumbu sahihi ya mkutano wa 14 wa Mwaka kwa kuazimia kama ifuatavyo

> **"Azimio la 2/2020**
>
> **Imeazimiwa kuwa Muhtasari wa Mkutano wa kumi na Nne uliofanyika tarehe 10 Agosti 2019 ni kumbukumbu sahihi"**



## YATOKANAYO NA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA KUMI NA NNE TEREHE 10 AGOSTI 2019

| Kumb. | Maelezo Mafupi | Azimio | Utekelezaji |
|---|---|---|---|
| 14.10.1 | Kustaafu kwa Afisa Mtendaji Mkuu na Mhasibu wa Kampuni | Wajumbe waliazimia Bodi kuangalia namna ya kumpongeza Afisa Mtendaji wa Kampuni, Ndugu Donald J. Kamori na Mhasibu wa Kampuni, Ndugu, Edgar L. Kahabwa wanaomaliza muda wao katika kuitumikia Kampuni kwa kazi nzuri. | Agizo limetekelezwa Bodi iliwanunulia hati fungani (government bonds) zenye thamani ya shilingi milioni 100. |



**Dondoo Na. 15/6/2020**

## TAARIFA YA MWENYEKITI MWAKA 2019

### 1. UTANGULIZI

Ndugu Wanahisa, ninayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2019. Kwa mwaka 2019, Kampuni ilipata mafanikio makubwa kutokana na hatua madhubuti zilizochukuliwa na Bodi na Menejimenti pamoja na usimamizi mzuri ambao umechangia ongezeko la thamani kwa wanahisa. Kampuni ilifanya mikakati ya kuainisha maeneo mengine mapya ya uwekezaji wa muda mrefu katika taasisi ya fedha na kuomba mkopo benki ambapo umewekezwa katika Amana za Serikali (Government Bond).

### 2. BIASHARA ENDELEVU

Kampuni ina malengo ya muda mrefu katika kutimiza maono yake, dhima na maadili ya msingi yanayojumuisha Nyanja tatu ambazo ni: Ongezeko la thamani kwa Wanahisa, ubora wa uwekezaji, na ubora katika utendaji. Kampuni kuendelea na shughuli zake za biashara ni mojawapo ya fursa kubwa ambayo tunaamini kwa kufanya kazi pamoja kwa kushirikiana na wadau wetu wakuu kunaweza kuleta ufanisi zaidi na mazingira salama ya kiutendaji. Uimara wa Kampuni ni nguzo muhimu katika utendaji na kutokana na malengo mapya tuliyonayo tutaweza kuchukua hatua madhubuti.

Licha ya dalili zilizojitokeza za kupungua kwa mauzo katika Soko la Hisa, kushuka kwa thamani ya hisa, kutofanya vizuri kwa makampuni ambayo TICL imewekeza, bado Kampuni imeendelea kuchukua hatua stahiki na kupata faida. Kuwa na uwezo wa kutengeneza faida hata katika mazingira magumu ni moja ya malengo mapya ya kifedha ambayo yameainishwa katika Mpango Mkakati wa Kampuni kwa mwaka 2020 - 2022. Kampuni ina mpango wa kuwekeza katika vyanzo mbalimbali vya mapato na kuacha kutegemea chanzo kimoja ili kuimarisha mapato. Tunalenga kuongeza faida kwa asilimia 22 kwa mwaka.

### 3. GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Disemba 31, 2019, Bodi inapendekeza malipo ya gawio yawe Shilingi 6 kwa hisa moja ukilinganisha na Shilingi 2.54 kwa hisa moja kwa mwaka 2018. Malipo ya gawio yaliyopendekezwa yanategemea kuidhinishwa na wanahisa wakati wa Mkutano Mkuu wa 15 utakaofanyika mnamo 22 Agosti 2020.

### 4. MATARAJIO YA BAADAE

Mipango ya baadaye ni pamoja na kuimarisha ongezeko la thamani kwa wanahisa, kukuza uwekezaji na kuongeza mapato ya uwekezaji na kuboresha utendaji kwa kuimarisha nguvu kazi na matumizi ya teknolojia kama vile kufanya malipo kwa njia ya mtandao. Tunalenga kuwekeza katika maeneo mapya ya uwekezaji kama vile usindikaji na uhifadhi wa mazao ya kilimo, korosho, kusimamia shughuli za uwekezaji, huduma za kifedha na kujenga maghala ya kuhifadhia nafaka.

### 5. SHUKURANI

Mwisho, kwa niaba ya Bodi, tunapenda kutoa shukrani zetu za dhati kwa Wanahisa wetu wote, wateja na washirika wetu katika biashara. Napenda pia kuwashukuru Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE) na mamlaka zingine kwa msaada na mwongozo wao mzuri. Nawashukuru pia

Bodi ya Wakurugenzi kwa juhudi zao katika kuiwezesha kampuni kuendelea kufanya vizuri na utekelezaji wa Mpango Mkakatati mwaka tuliojiwekea.

Kwa niaba ya Bodi, napenda nimshukuru Ndugu Donald J. Kamori ambaye amestaafu kuwa Afisa Mtendaji Mkuu na Katibu wa Bodi kwenye Kampuni yetu toka tarehe 31 Desemba, 2019. Tuna deni kwake kwa miaka 14 aliyofanya kazi kwenye Kampuni kama Afisa Mtendaji Mkuu, tangu mwaka 2005. Tunamtakia kila la kheri katika majukumu yake ya kila siku.

Napenda pia kumkaribisha Ndugu Peter W. Kifunguomali ambaye aliteuliwa kama Afisa Mtendaji Mkuu mpya kuanzia tarehe 1 Januari, 2020. Kwa niaba ya Bodi, napenda kuishukuru Menejimenti kwa kusimamia vema na kuweza kutekeleza vipaumbele vilivyowekwa na Bodi. Ninawashukuru pia wafanyakazi wetu wote wa kampuni kwa kufanya kazi kwa bidii na kujitoa ili kuongeza mapato na ongezeko la thamani kwa Wanahisa.
Mwisho kabisa, napenda kutoa shukrani zetu kwa Wanahisa kwa kuendelea kuwa pamoja nasi na kuiamini Kampuni. Tunapoendelea na safari hii, nina imani kuwa kwa pamoja tunaweza kufanya vizuri zaidi. Kwa Wanahisa na wadau wetu wote, tunasisitiza kuendelea kujitoa na kuongeza juhudi katika kazi.

Asanteni Sana

Fortunatus M. Magambo
Mwenyekiti wa Bodi

**Dondoo Na. 15/6/2020**

# TAARIFA YA AFISA MTENDAJI MKUU KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA DISEMBA 31, 2019.

## 1. UTANGULIZI

Kwa mwaka ulioishia Desemba 31, 2019, tumepiga hatua kubwa sana. Mapato yameongezeka kwa asilimia 24.55 wakati gharama za uendeshaji zikipungua kwa asilimia 5.6. Tumefanikiwa kuongeza gawio kwa asilimia 136. Bodi imeandaa Mpango Mkakati mpya wa miaka mitatu ili kuweza kusimamia shughuli za Kampuni katika maeneo muhimu manne kama: Ufanisi wa huduma, kuongeza faida, kurahisisha mzunguko wa fedha na kuongeza mapato. Hii inaendana na mipango ambayo iliwasilishwa kwa mwaka huu ya kuimarisha ongezeko la thamani kwa Wanahisa wa Kampuni ikiwa ni pamoja na kuimarisha ongezeko la thamani ya hisa, ubora wa uwekezaji na ubora wa huduma za kiutendaji. Tunaendelea kukuza ongezeko la thamani la muda mrefu kwa wanahisa na kuimarisha uwekezaji kulingana na ushindani. Tumefanya maamuzi kadhaa muhimu katika kutekeleza hili ikiwa ni pamoja na kuomba mkopo kutoka Benki ili kuwekeza katika maeneo yenye faida kubwa.

## 2. UCHAMBUZI WA THAMANI INAYOTOKANA NA UWEKEZAJI.

Kampuni yetu tangia kuanzishwa kwake imekua ikifanya uwekezaji makini na wenye kuleta tija hivyo kuwezesha kukuza thamani ya mtaji kutoka shilingi 2,000 milioni mwaka 2005 hadi kufikia shilingi 29,500 milioni mwaka 2019 kwa kuwekeza maeneo mbali mbali ikiwamo Kwenye hisa za makampuni mengine pamoja na amana za Serikali. Kwa mwaka 2019 pekee kampuni imefanikiwa kupata mrejesho kutokana na uwekezaji wa asilimia 36 kwa kuzingatia mapato, na asilimia 137 kwa kuzingatia ongezeko la thamani (capital gain). Kampuni imekua ikipata faida na kutoa gawio kwa wanahisa wake bila kuacha kuanzia mwaka 2012.

## 3. TAARIFA YA KIUTENDAJI

Kampuni imeendelea kufanya vizuri kwenye Mapato, kutengeneza faida, uwekezaji, ongezeko la thamani ya hisa n.k. Mapato mengine ya mwaka 2019 ukilinganisha na taarifa ya 2018 imeonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

| MAELEZO | KIPIMO | MWAKA 2019 | MWAKA 2018 |
|---|---|---|---|
| Mapato | Shilingi '000' | 1,787,692 | 1,435,266 |
| Gharama za Uendeshaji wa Kampuni. | Shilingi '000' | 1,061,732 | 1,125,208 |
| Faida baada ya Kukata Kodi | Shilingi '000' | 409,714 | 422,391 |
| Mali za wanahisa | Shilingi '000' | 27,096,381 | 28,374,783 |
| Thamani ya kila hisa (mali ukiondoa madeni). | Shilingi | 371 | 388 |
| Mapato kwa kila hisa. | Shilingi | 5.62 | 5.78 |
| Gawio kwa kila hisa | Shilingi | 6 | 2.54 |

## UCHAMBUZI WA UWEKEZAJI KWA MWAKA 2019

Kwa mwaka 2019, kazi kubwa iliyofanywa na Kampuni ni kuwekeza katika maeneo mbalimbali. Kampuni iliwekeza jumla ya Shilingi 5.43 bilioni kwenye Amana za Serikali (Government Bonds). Kampuni ilinunua Amana za Serikali za miaka 15 zenye faida ya asilimia 13.5 na miaka 20 zenye faida ya asilimia 15.49. Kampuni iliuza hisa zenye thamani ya Shilingi 1.88 bilioni, pia ilichukua mkopo wa shilingi 3 bilioni kutoka CRDB kama moja ya mkakati wake wa kuwekeza kwenye vyanzo vingine vya mapato. Kwa mwaka 2019, ilibadili uwekezaji kutoka chanzo kimoja cha mapato kwenda kwenye vyanzo vingine kwa kuzingatia Kanuni ya Kampuni na Sera ya Uwekezaji. Maeneo ambayo Kampuni imewekeza ni Pamoja na Amana za serikali, Amana za Makampuni, Amana za mabenki, Hisa na uwekezaji kwenye mali zisizohamishika. Kufikia Disemba 31, 2019, uwekezaji uliongezeka kwa asilimia 4.8 na kufikia Shilingi 29.53 bilioni ukilinganisha na Shilingi 28.18 bilioni kwa mwaka 2018.

Maeneo ambayo Kampuni iliwekeza kufikia Desemba 31, 2019 kwa muhtasari ni kama ilivyoainishwa kwenye jedwali hapa chini:

| Aina ya uwekezaji | 2019 (Sh milioni) | % ya Uwekezaji | 2018 (Shs milioni) | % ya Uwekezaji | Ongezeko/Pungufu (Sh milion) |
|---|---|---|---|---|---|
| Hisa | 19,364.88 | 65.58% | 22,988 | 81.59% | (3,623.12) |
| Amana za serikali | 9,677.92 | 32.77% | 4,249.24 | 15.08% | 5,428.68 |
| Amana za Benki | 210 | 0.71% | 634.2 | 2.25 | (424.2) |
| Amana za makampuni | 30.34 | 0.1% | 58.71 | 0.21% | (28.37) |
| Mali zisizohamishika | 239.82 | 0.81% | 239.82 | 0.85% | - |
| Maeneo Mengine | 5.5 | 0.02% | 5.5 | 0.02% | - |
| **Jumla ya Uwekezaji** | **29,528.46** | | **28,175.47** | | **1,352.99** |

Tuna imani ya kukamilisha malengo tuliyojiwekea kufikia mwishoni mwa mwaka huu wa 2020 na kupata faida kati ya asilimia 15 hadi 20 (15% - 20%). Japokuwa Soko halifanyi vizuri, bado Kampuni imeendelea kufanya vizuri, na kutuweka kwenye nafasi nzuri katika ushindani wa uwekekezaji. Kwa mwaka huu wa 2020 tunategemea pia kupata faida.

**Gawio** limeongezeka kwa **136%**

**Ongezeko** la thamani Mtaji **137%**

## MPANGO WA KAMPUNI KWA MWAKA 2020-2022

Kufikia mwaka 2022, tunategemea kuwa Kampuni itakuwa moja ya kituo kikuu cha kusimamia uwekezaji Tanzania kwa kutengeneza ongezeko la thamani kwa wanahisa kwa faida itakayotokana na uwekezaji safi na salama. Kampuni inalenga kuunda Kampuni tanzu na kugawanya uwekezaji wake kwa asilimia 50:50 kutoka kwenye uwekezaji wa sasa ifikapo mwaka 2022. Kampuni tayari imefanya hatua madhubuti za kuongeza mapato ya uwekezaji kwa asilimia 68 ifikapo Disemba 2022. Ili kufikia lengo hili, Kampuni ina mpango wa kuongeza ubora wa kiutendaji kwa uwiano wa asilimia 95.

Wakati huu Kampuni ikiendelea kukua, pia tutaendelea kulinda utawala bora na usimamizi wa athari zinazoweza kujitokeza.

Mwisho, nachukua fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa wanahisa wote, Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti, mabenki, Wakaguzi wa mahesabu na Wawekezaji kwa kujitoa kwao bila kuchoka kusaidia Kampuni yetu.

Asante Sana



...............................................

Peter William Kifunguomali

Afisa Mtendaji Mkuu

Tarehe:

## TAARIFA YA WAKURUGENZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DISEMBA, 2019

### UTANGULIZI

Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kuwasilisha Taarifa ya Wakurugenzi pamoja na Taarifa ya Mahesabu yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2019. Taarifa hii inatoa picha kamili ya hali halisi ya Kampuni.

### UANZISHWAJI WA KAMPUNI

Kampuni ilianzishwa Novemba, 1999 na kuanza shughuli za biashara Januari, 2005. Kampuni inafanya biashara kwa njia ya Uwekezaji wa pamoja ambapo wanachama wa TCCIA waliweza kukusanya mtaji kwa lengo la kununua hisa za NMB kupitia agizo la Serikali la kutaka kuibinafsisha.

Kufikia Disemba 31, 2018, jumla ya wanahisa walikuwa 3,426 ambapo PSSSF ni shirika pekee ambalo linamiliki asilimia 38.5 ya hisa zote za Kampuni. Wanahisa waliobaki ni watu binafsi na baadhi ya makampuni madogo na ya kati.

### BIASHARA YA KAMPUNI

Kulingana na Katiba ya Kampuni (MEMARTS), biashara kuu ya Kampuni ni uwekezaji katika viwanda, taasisi za fedha, huduma za mawasiliano, kilimo, madini, ujenzi wa barabara, ujenzi wa majengo na huduma za kijamii.

### MAONO, DHIMA, KAULI MBIU NA MAADILI KATIKA KAZI

Maono, Dhima Maadili katika kazi ni kama ifuatavyo:-.

#### MAONO YA KAMPUNI

"Kuwa kituo kikuu cha usimamizi wa uwekezaji Tanzania.

#### DHIMA YA KAMPUNI

Kutengeneza ongezeko la thamani ya muda mrefu kwa wanahisa wa Kampuni kwa kutoa faida nzuri zaidi inayotokana na uwekezaji bora na salama.

#### KAULI MBIU

Kwa pamoja tunaweza.

#### MAADILI KATIKA KAZI:

Uwajibikaji, Kujitoa, Kufanya kazi kwa pamoja, Uaminifu na uvumbuzi.

### DHUMUNI NA MPANGO MKAKATI WA KAMPUNI;

Ongezeko la Thamani: Kuiwezesha Kampuni kufikia lengo la wanahisa la kuanzishwa kwa hii Kampuni. Lengo kuu ni kuongeza thamani ya Hisa na kukuza mtaji wa Kampuni. Kampuni pia inalenga kuanzisha Kampuni tanzu ili kugawanya mtaji wake katika maeneo mengine ya biashara.

**UWEKEZAJI BORA:** Kampuni ina lengo la kuimarisha thamani ya Kampuni kwa kuimarisha rasilimali za Kampuni na kuongeza kipato katika uwekezaji. Kampuni ina mpango wa kukuza kipato kupitia uwekezaji kwa asilimia ishirini na mbili (22%) kwa mwaka.

**UTENDAJI BORA:** Kampuni ina mpango wa kuimarisha utendaji kupitia wafanyakazi waliopo na teknolojia ili kukuza ufanisi, kuhudumia wanahisa, kukidhi matakwa ya mamlaka zinazoisimamia, kuimarisha utamaduni wa ushirikiano, kuimarisha maslahi ya wafanyakazi na kuimarisha utendaji na uwajibikaji wa wafanyakazi. Kampuni ina mpango wa kufanikisha mipango yake kwa asilimia tisini na tano (95%).

## BIASHARA ENDELEVU

Katika majadiliano ya Bodi katika kuimarisha ukuaji wa Kampuni, haukuzingatia kushuka na kupanda kwa thamani ya fedha. Bodi ilizingatia kulinda na kuhakikisha Kampuni inaendeleza utendaji wake, mabadiliko ya tabia nchi na rasilimali zinazohitajika ili Kampuni iendelee kufanikiwa kwa miaka ijayo. Lakini pia tunaamini katika kuimarisha mazingira ya utendaji katika kuepuka kuwekeza kwenye miradi ambayo itaharibu sifa nzuri ya Kampuni hata kama utakuwa na faida kubwa; kuhimiza wafanyakazi na wadau wa Kampuni kujiendeleza, kujizoeza na kutumia teknolojia, kutumia mtandao, kuongeza upeo wa wafanyakazi wa TICL katika utendaji na kuwahimiza wadau wa Kampuni kuhusu kuondoa madhara ya kimfumo kupitia teknolojia,

## WAKURUGENZI WA KAMPUNI

Kwa mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2019, Wakurugenzi walikuwa hawa wafuatao:

| JINA | NAFASI | KUZALIWA | URAIA | SIFA/ELIMU | TAREHE YA KUJIUNGA NA KAMPUNI |
|---|---|---|---|---|---|
| Bwn. Fortunatus Magambo | Mwenyekiti | 1969 | Mtanzania | Mchumi | 10.08.2019 |
| Prof. Lucian A. Msambichaka | Makamu Mwenyekiti | 1943 | Mtanzania | Mchumi | 10.08.2019 |
| Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 1964 | Mtanzania | Mhasibu | 10.08.2019 |
| Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 1954 | Mtanzania | Kilimo/Mchumi | 10.08.2019 |
| Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 1968 | Mtanzania | Mchumi | 10.08.2019 |
| Bwn. Peter W. Kifunguomali* | Mjumbe | 1981 | Mtanzania | Mchumi | 10.08.2019 |
| Bwn. Octavian Mshiu* | Mjumbe | | Mtanzania | Mfanyabiashara | 10.08.2019 |
| Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 1966 | Mtanzania | Mauzo na Manunuzi | 02.09.2019 |
| Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe | 1961 | Tanzanian | Teknohama | 30.09.2019 |

## MABADILIKO KWENYE BODI

*Kufikia mwezi Agosti, 2019 Bwana Peter W. Kifunguomali, ambaye alikuwa anawakilisha Mfuko wa Hifadhi ya jamii (PSSSF) alistaafu kuwa Mjumbe wa Bodi na nafasi yake kuchukuliwa na Bwana Ernest R. Khisombi.

*Kufikia mwezi August, 2019, Bwana Octavian Mshiu, ambaye alikuwa anawakilisha Ofisi ya TCCIA Makao Makuu pamoja na Matawi yake yaliyopo mikoa yote ya Tanzania katika nafasi ya Rais, alistaafu kuwa mjumbe wa Bodi na nafasi yake kuchukuliwa na Bwana Paul R. Koyi.

## UTAWALA BORA

Kanuni ya Kampuni inaitaka Bodi kuwa na Wajumbe saba (7) na wasipungue watano (5). Mwaka 2019, wajumbe wa Bodi walikuwa saba (7). Hakuna Mjumbe yoyote wa Bodi ambaye ni mfanyakazi wa Kampuni. Bodi inasimamia shughuli zote za Kampuni. Pamoja na mambo mengine, Bodi inaainisha athari zinazoweza kujitokeza katika shughuli za Kampuni, kutafuta njia za kuzuia katika kufanya maamuzi ya uwekezaji. Bodi inahakikisha taratibu zote katika utendaji wa Kampuni zipo na zinafuatwa kulingana na kanuni za utawala bora.

Kwa mwaka wa fedha ulioishia Disemba 31, 2019, Bodi ilikutana mara sita (6), ambapo Vikao vya kawaida vilikuwa vinne (4) na vikao maalum viwili (2). Shughuli za kila siku za Kampuni zinasimamiwa na Afisa Mtendaji Mkuu akisaidiwa na wafanyakazi walioko chini yake. Menejimenti pia huwa inaalikwa kuhudhuria vikao vya Bodi ili kuimarisha ufanisi katika shughuli za Kampuni na Utawala bora. Lengo la kufanyika kwa vikao maalum, ni pamoja ya kujadili na kuidhinisha taarifa ya mahesabu ya kampuni yaliyokaguliwa.

### WAJUMBE WA BODI KWA MWAKA 2019, NA IDADI YA VIKAO WALIVYOHUDHURIA.

| Na. | Jina | Nafasi | IdadiyaVikao | Idadi ya Vikao Alivyohudhuria |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Bwn.FortunatusMagambo | Mwenyekiti | 6 | 6 |
| 2. | Prof.Lucian A. Msambichaka | MakamuMwenyekiti | 6 | 6 |
| 3. | Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mjumbe | 6 | 6 |
| 4. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe | 6 | 6 |
| 5. | Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe | 6 | 3 |
| 6. | Bwn. Peter W. Kifunguomali* | Mjumbe | 6 | 4 |
| 7. | Bwn. Octavian Mshiu* | Mjumbe | 6 | 2 |
| 8 . | Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe | 6 | 1 |
| 9. | Bwn. Ernest R. Khisombi | Mjumbe | 6 | 2 |

Wajumbe wote wa Bodi wana sifa na uzoefu unaojitegemea ambao unasaidia katika kufanya maamuzi. Wajumbe wote hufuata Utawala Bora katika kufanya maamuzi.

Wajumbe wa Bodi wanatambua na kufuata Kanuni za Utawala Bora. Kwa mwaka wa fedha wa 2019, ili kutimiza kanuni za Utawala Bora, Bodi iliunda kamati mbili ambazo zilikutana kujadili mambo yahusianayo na shughuli za Kampuni. Kamati hizo ni:-

- Kamati ya Uwekezaji ambayo ina wajumbe watatu.
- Na kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ambayo ina wajumbe watatu.

| | WAJUMBE WA KAMATI YA UWEKEZAJI: | |
|---|---|---|
| 1. | Prof. Lucian A. Msambichaka | Mwenyekiti |
| 2. | Bwn. Nathan E. Mnyawami | Mjumbe |
| 3. | Bwn. Paul F. Koyi | Mjumbe |

Kamati ya Uwekezaji ilikutana mara nne (4) kujadili taarifa ya Kampuni ya kila robo mwaka, Taarifa ya Upembuzi Yakinifu na Mpango Mkakati na Bajeti ya Kampuni kabla ya kuwasilisha kwenye Bodi kwa majadiliano na kufanya maamuzi.

**WAJUMBE WA KAMATI YA UKAGUZI NA KUZUIA ATHARI KATIKA KAMPUNI: -**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Bwn. Joseph M. Kahungwa | Mwenyekiti |
| 2. | Bwn. Peter W. Kifunguomali | Mjumbe |
| 3. | Bi. Magdalene N. E. Mkocha | Mjumbe |

Kamati ya Ukaguzi na Kuzuia Athari katika Kampuni ilikutana mara sita (6) kujadili Taarifa ya ndani ya Kampuni inayoandaliwa na Mkaguzi wa ndani na pia kupitia mahesabu ya Kampuni ya Mwaka mzima kabla na baada ya kukaguliwa.

## MAJUKUMU YA BODI KWA MWAKA 2019

Pamoja na Kusimamia shughuli za Bodi kwa mwaka 2019, Bodi ina majukumu yafuatayo:-

- Kuandaa Mpango Mkakati wa Kampuni kwa Mwaka 2020-22;
- Kuhakiki Taarifa za wanahisa wa Kampuni;
- Kupitia taarifa ya Kampuni iliyoandaliwa na Mkaguzi wa ndani;
- Kutafuta njia mbalimbali za kupunguza gharama za uendeshaji wa Kampuni na kuongeza mapato;
- Kuandaa mpango mkakati na kupitisha bajeti ya mwaka 2020.
- Kufanya Upembuzi yakinifu na kukuza mapato ya Kampuni.

Idadi ya Hisa zinazomilikiwa na Wajumbe wa Bodi kwenye Kampuni

Idadi ya Hisa za kila Mjumbe wa Bodi ni kama ifuatavyo: -

| NA. | JINA | IDADI YA HISA ANAZOMILIKI |
|---|---|---|
| 2. | Prof. Lucian Ambrose Msambichaka | 487,580 |
| 5. | Bwn. Joseph Matanga Kahungwa | 40,600 |
| 6. | Bwn. Nathan Edward Mnyawami | 19,675 |

| Na. | Jina | Idadi ya Hisa Anazomiliki |
|---|---|---|
| 8. | Bi. Magdalene Nelson Enock Mkocha | 102,363 |
| 9. | Bwn. Octavian E. Mshiu ** | 830,498 |
| 10. | Bwn. Fortunatus Magambo** | |
| 11. | Bwn. Peter W. Kifunguomali** | 28,100,300 |

**Bwana Octavian E. Mshiu: Alihudumu kwenye Bodi kwa mwaka 2019 katika nafasi yake ya kukaimu nafasi ya Raisi wa TCCIA ya kuiwakilisha TCCIA Makao Makuu ya Ofisi za Matawi yake zilizoko Mikoa yote ya Tanzania ambao wanamiliki jumla ya Hisa 830,213. Hata hiyo katika uchaguzi wa TCCIA uliofanyika mwaka 2019 walimchagua Bwana Paul Koyi kujaza nafasi ya Raisi ilyokuwa wazi.

**Bwana Fortunatus Magambo na Bwana Peter William Kifunguomali kwa pamoja wanawakilisha Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (PSSSF) unaomiliki jumla ya Hisa 28,100,300. Kufuatia Bwana Peter W. Kifunguomali kustaafu kuwa mjumbe wa Bodi, nafasi yake ilichukuliwa na Bwana Ernest R. Khisombi.


















## Bodi ya Wakurugenzi

1. **Fortunatus Magambo**
   Mwenyekiti
2. **Mr. Mnyawami**
   Mjumbe
3. **Prof. Lucian Ambrose Msambichaka**
   Mjumbe
4. **Bi Magdalene Nelson Enock Mkocha**
   Mjumbe
5. **Bwn. Joseph Matanga Kahungwa**
   Mjumbe
6. **Bwn. Paul Faraj Koyi**
   Mjumbe
7. **Bwn. Ernest R. Khisombi**
   Mjumbe
8. **Bwn. Peter W. Kifunguomali**
   Afisa Mtendaji Mkuu / Katibu

## MTAJI WA KAMPUNI

Mtaji wa Kampuni ulioidhinishwa ni Shilingi 100,000,000,000 ambao imegawanywa kwa mfumo wa hisa ambapo kufikia Desemba 31, 2019 thamani ya hisa moja ilikuwa sawa na Shilingi 20. mpaka kufikia Desemba 31, 2019 hisa zilizokuwa zimelipiwa ni sawa na Shilingi 2.16 bilioni.

## MGAWANYO WA MTAJI WA KAMPUNI NA UMILIKI WAKE

Kufikia Desemba 31, 2019, idadi ya Wanahisa ilikuwa 3,426 ambapo haina tofauti na idadi ya Wanahisa kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 31 Disemba, 2018. Mgawanyiko huu wa hisa za Kampuni na kama inavyoonyeshwa kwenye jedwali hapa chini:

| | 2018 | 2019 | 2018 | 2019 | 2018 | 2019 | 2018 | 2019 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Up to 28,100,300 | 1 | 1 | 38.50% | 38.50% | 28,100,300 | 28,100,300 | 562,006,000.00 | 562,006,000.00 |
| 1,700,001 -4,300,000 Shares | 1 | 1 | 5.80% | 5.80% | 4,215,000 | 4,215,000 | 84,300,000.00 | 84,300,000.00 |
| 1,600,001 -1,700,000 Shares | 1 | 1 | 2.30% | 2.30% | 1,686,000 | 1,686,000 | 33,720,000.00 | 33,720,000.00 |
| 1,250,001-1,600,000 Shares | 1 | 1 | 1.90% | 1.90% | 1,405,000 | 1,405,000 | 28,100,000.00 | 28,100,000.00 |
| 1,200,001 -1,250,000 Shares | 1 | 1 | 1.70% | 1.70% | 1,236,400 | 1,236,400 | 24,728,000.00 | 24,728,000.00 |
| 800,001 -1,200,000 Shares | 1 | 1 | 1.50% | 1.50% | 1,123,975 | 1,123,975 | 22,479,500.00 | 22,479,500.00 |
| 600,001 -800,000 Shares | 1 | 1 | 0.90% | 0.90% | 674,375 | 674,375 | 13,487,500.00 | 13,487,500.00 |
| 300,001 -600,000 Shares | 7 | 7 | 3.70% | 3.70% | 2,692,424 | 2,692,424 | 53,848,480.00 | 53,848,480.00 |
| 100,001 -300,000 Shares | 52 | 52 | 11.97% | 11.97% | 8,746,222 | 8,746,222 | 174,924,440.00 | 174,924,440.00 |
| 50,001 -100,000 Shares | 117 | 117 | 9.60% | 9.60% | 7,048,046 | 7,048,046 | 140,960,920.00 | 140,960,920.00 |
| 20,001 -50,000 Shares | 168 | 168 | 6.70% | 6.70% | 4,872,576 | 4,872,576 | 97,451,520.00 | 97,451,520.00 |
| 10,001 -20,000 Shares | 297 | 297 | 5.60% | 5.60% | 4,079,546 | 4,079,546 | 81,590,920.00 | 81,590,920.00 |
| 5,001 -10,000 Shares | 535 | 535 | 4.60% | 4.60% | 3,338,308 | 3,338,308 | 66,766,160.00 | 66,766,160.00 |
| 1,001 -5,000 Shares | 1508 | 1508 | 4.90% | 4.90% | 3,596,198 | 3,596,198 | 71,923,960.00 | 71,923,960.00 |
| 501 -1,000 Shares | 143 | 143 | 0.20% | 0.20% | 131,170 | 131,170 | 2,623,400.00 | 2,623,400.00 |
| 101 -500 Shares | 377 | 337 | 0.20% | 0.20% | 110,474 | 110,474 | 2,209,480.00 | 2,209,480.00 |
| 51 -100 Shares | 212 | 212 | 0.03% | 0.03% | 20,150 | 20,150 | 403,000.00 | 403,000.00 |
| 1-50 Shares | 3 | 3 | 0.00% | 0.00% | 92 | 92 | 1,840.00 | 1,840.00 |

## MTAJI WA KAMPUNI NA UMILIKI WAKE

| DONDOO | 2019 "SHILINGI" | 2018 "SHILINGI" |
|---|---|---|
| Mtaji Ulioidhinishwa (Sh 20 kwa hisa 5,000,000,000) | 100,000,000,000 | 100,000,000,000 |
| Mtaji Uliolipiwa (Shs 20 kwa hisa 72,957,660) | 1,459,153,000 | 1,459,153,000 |
| Mtaji uliolipiwa Zaidi (Share premium) | 708,799,000 | 708,799,000 |

Utendaji katika Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 31 Desemba, 2019. Kwa mwaka 2019, faida ya kampuni ilipungua kwa asilimia 3 hadi kufikia shilingi 409,714,000 ukilinganisha na mwaka 2018.

**Mapato ya Kampuni yaliongezeka**
**25%**

**Kufikia Desemba 31, 2019, idadi ya Wanahisa ilikuwa**
**3,426**


Mapato ya Kampuni yaliongezeka kwa asilimia 25% na kufikia Shilingi 1,787,692,000 ukilinganisha na mwaka 2018. Ongezeko hili linatokana na uamuzi wa Bodi wa kuuza baadhi ya hisa zinazomilikiwa na Kampuni za Makampuni mengine na kuwekeza katika vyanzo vingine vya mapato ikiwamo Amana za Serikali (Government Bonds) kwa mwaka 2018 na 2019.

## KULIPA GAWIO

Kwa mwaka wa fedha 2019 bodi inapendekezeza gawio la shilingi 6 kwa hisa (2018: shilingi 2.54).

## USAWA WA KIJINSIA KAZINI

Kampuni inazingatia usawa wa kijinsia katika kuajiri wafanyakazi wake na haina ubaguzi katika utendaji wake. Kufikia Desemba 31, 2019, wafanyakazi wa Kampuni walikuwa kama ilivyoainishwa na jinsia zao kwenye jedwali hapa chini:




| | 31 - DIS | 31 - DIS |
|---|---|---|
| Jinsia | 2019 | 2018 |
| Wanaume | 4 | 3 |
| Wanawake | 2 | 2 |
| Jumla | 6 | 5 |

## MASLAHI YA WAFANYAKAZI

Kampuni inawapa wafanyakazi wake maslahi yafuatayo:

### ELIMU

Kampuni inawafadhili wafanyakazi wake kujiendeleza kielimu katika kozi za muda mfupi ndani na nje ya nchi kwa taaluma mbalimbali kulingana na uhitaji na kiwango cha fedha kinachohitajika. Kampuni pia inasaidia wafanyakazi pale wanapoamua kujiendeleza wenyewe kwa masomo ya muda mrefu.

### MKOPO KWA WAFANYAKAZI.

Kampuni inatoa mikopo kwa wafanyakazi ya muda mrefu na mfupi kuweza kutatua matatizo ya kifedha na kufanya shughuli nyingine za kiuchumi za kujiongezea kipato. Mikopo hiyo inatolewa kulingana na masharti yaliyowekwa na Bodi na inatolewa kulingana na Bajeti ya mwaka.

### HUDUMA YA MATIBABU

Kampuni imeingia mkataba na Shirika la Bima ya Afya la Taifa (NHIF) kutoa huduma ya afya kwa wafanyakazi wa Kampuni na wategemezi wao.

### MSAADA WA KIFEDHA

Kampuni inaandaa sera ya kusaidia pale mfanyakazi anapofariki au wategemezi.

### MAFAO YA KUSTAAFU

Kampuni inachangia kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii (PSSSF na NSSSF) kwa ajili ya mafao ya baadaye kwa wafanyakazi wake.

### WATU WASIOJIWEZA (WALEMAVU WA VIUNGO)

Kampuni inatoa nafasi sawa ya ajira kwa watu wote yaani wenye viungo vyote na wale wenye ulemavu wa viungo.

### KUKIDHI MATAKWA YA KISHERIA

Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na wadau wake. Lakini pia Kampuni imeendelea kuwa na uhusiano mzuri na mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), mamlaka ya Usimamizi wa Mitaji na Dhamana (CMSA), Soko la Hisa (DSE), Madalali wa Soko la Hisa (Brokers) na benki za Biashara. Kwa mwaka 2019, Kampuni imeweza kutimiza taratibu na vigezo vyote kulingana na Matakwa ya Mamlaka husika.

### UDHIBITI WA ATHARI ZA UTAWALA WA NDANI YA KAMPUNI

Bodi ina wajibu wa kudhibiti athari zinazoweza kujitokeza katika utendaji kwenye Kampuni. Menejiment inahakikisha kuwa kunakuwa na fedha za kutosha na mfumo wa ufanyaji kazi katika Kampuni unazingatiwa. Lengo la Kampuni ni:

- Kulinda stahiki za wanahisa na mali ya Kampuni.
- Ufanisi na Ubora katika kazi;
- Kukidhi matakwa ya Mamlaka na Sheria.
- Kuwepo kwa rekodi ya Mahesabu na Taarifa ya Fedha.
- Kampuni kuendelea na shughuli za utendaji katika mazingira ya kawaida na yasiyo ya kawaida.
- Kuwajibika kwa wadau wa Kampuni.

Ufanisi na udhibiti wa mfumo wowote wa utendaji wa ndani unategemea utaratibu wa hatua zilizochukuliwa. Kuna athari zinazoweza kujitokeza kwa kushindwa kufuata taratibu zilizowekwa kwa wafanyakazi. Mfumo wa ndani wa Kampuni una lengo la kuwahakikishia wakurugenzi, kazi zinafanyika kwa ufanisi. Wakurugenzi wana mamlaka ya kufuatilia mfumo wa ndani wa utendaji na kujiridhisha.

Kampuni ina sera mbalimbali ambapo kupitia hizo inaweza kudhibiti athari kwenye Kampuni. Na kwa upande mwingine, Kampuni imemwajiri Mkaguzi wa ndani wa muda ambaye anasimamiwa na Bodi kupitia Kamati ya Ukaguzi ambapo kupitia yeye Bodi inaweza kusimamia utendaji wa Kampuni kwa ufanisi mkubwa.

## TATHMINI NA ATHARI ZA KAMPUNI NA NAMNA YA KUZIZUIA.

Kampuni imewekeza katika taasisi ya fedha ikiwemo Amana za serikali za muda mfupi na muda mrefu, Amana za Makampuni, mikopo, amana za mabenki na kwenye hisa. Maeneo mengine ya uwekezaji ni pamoja na biashara zinazotoa faida. Lengo la uwekezaji huu ni kuongeza mapato kwenye Kampuni.

Athari zinazoweza kuikumba kampuni ni pamoja na: -

## ATHARI YA KUTOKUPATA FAIDA

Hii inatokana na mwenendo wa Hisa katika Soko la Hisa ambao hisa za makampuni ambapo Kampuni inamiliki hisa zimeshuka thamani. Uwekezaji katika Amana za Serikali kipato chake ni cha uhakika na husaidia kupunguza athari ya kukosa faida katika Kampuni.

## ATHARI YA UBADILISHAJI WA FEDHA.

Hii ni athari inayojitokeza wakati wa ubadilishaji wa fedha za kigeni. Hii haiathiri sana Kampuni kwa sababu kwa sasa hatuna biashara inayotupelekea kubadili fedha.

## ATHARI ZA MIKOPO

Hii inatokana na upande mmoja kushindwa kutimiza wajibu wake wa kulipa deni kwa tarehe inayopangwa. Ili kupunguza hii athari, Kampuni imeandaa sera ya uwekezaji kutathmini kabla ya kufanya uwekezaji na ngazi za uidhinishaji katika kila eneo la uwekezaji.

## ATHARI YA HISA KUSHINDWA KUUZWA

Hii athari inatokana na kushindwa kufikia malengo. Lakini pia hii athari inatokana na kushindwa kuuza hisa kwa wakati na bei uliyokusudiwa. Kampuni inaweza kupunguza hii athari kwa kuwekeza kwenye amana za benki za muda mfupi zinazoweza kukamilisha mipango yake ya uwekezaji na matumizi ya ndani ya Kampuni. Kampuni imekuwa ikifanya makisio ya mapato na matumizi ya kila mwezi. Kampuni inategemea kipato chake kikubwa toka kwenye Magawio ya Makampuni inayomiliki hisa na maeneo mengine ilikowekeza.

## ATHARI ZA KIUTENDAJI

Hii inatokana na mfumo duni, usimamizi dhaifu, utendaji dhaifu, udanganyifu katika kazi, wizi na makosa mengine ya kibinadamu. Kampuni inajitahidi kuiepuka hii athari kwa kuweka mfumo mzuri wa usimamizi wa ndani wa Kampuni. Moja ya mbinu za kudhibiti ni pamoja na kufuata miongozo ya kiutendaji na taratibu zilizowekwa, sera na miongozo na kuajiri Mkaguzi wa ndani wa muda. Kusimamia athari za kiutendaji katika Kampuni ni muhimu katika shughuli za kila siku. Menejimenti, Mkaguzi wa Ndani wa muda, Kamati ya Uwekezaji, Kamati ya Ukaguzi na Bodi ya Wakurugenzi wanahusika kikamilifu katika usimamizi wa Kampuni.

## ATHARI YA RASILIMALI WATU.

Kulingana na uhalisia wa shughuli za Kampuni, inahitaji wafanyakazi wenye nidhamu na wenye maarifa maalum katika maeneo muhimu ya kiutendaji. Muundo wa Wafanyakazi wa Kampuni unaisaidia Kampuni kuingiza mapato makubwa. Ili kuhakikisha athari hii ya rasilimali watu inazuiwa, kampuni inahakikisha inawekeza kwa wafanyakazi wake, kupitia kuboresha maslahi yao kila mara.

## ATHARI YA KAMPUNI KUPOTEZA SIFA YAKE NZURI.

Kampuni ina wajibu wa kuhakikisha majukumu yake yanafanyika vizuri ili kulinda sifa yake katika makampuni yaliyoorodheshwa kwenye Soko la Hisa kulingana na sheria na taratibu husika. Katika kuhakikisha hili linafanyika, Bodi na Menejimenti inahakikisha inatimiza wajibu wake kwa kuzingatia sheria za utawala bora na kwa kuzingatia utendaji bora.

## KULINDA MALI ZA KAMPUNI.

Wakurugenzi wana wajibu wa kulinda mali ya Kampuni. Bodi imeidhinisha baadhi ya sera na kanuni lakini haizuiliwi na taratibu za fedha, sera ya uwekezaji ili kuimarisha mazingira ya utendaji wa ndani. Hizi sera zimekuwa zikifanyiwa marekebisho mara kwa mara kulingana na mabadiliko ya mazingira ya kiutendaji. Bodi ya Wakurugenzi inayo furaha kutoa taarifa kwamba hakuna udanganyifu wowote uliofanyika kwa mwaka wa fedha wa 2019.

## UPATIKANAJI WA TAARIFA YA MAHESABU NA TAARIFA YA FEDHA.

Kampuni inayo wafanyakazi wenye uzoefu katika kitengo cha uhasibu na fedha. Vitabu vya mahesabu vimekuwa vikitunzwa na taarifa ya fedha inaandaliwa kulingana na Sheria ya Kimataifa ya Uandaaji wa taarifa za Mahesabu. (IFRS).

## MIPANGO YA BAADAYE.

Kuanzia mwaka 2018, Bodi ya Wakurugenzi iliamua kupunguza uwekezaji wake kwenye hisa na kuwekeza maeneo mengine ambayo ilikuwa bado haijawekeza. Toka Kampuni imeanza kufanya shughuli za biashara Oktoba, 2005 zaidi ya asilimia tisini na tano (95%) ya uwekezaji wake ilikuwa ni kwenye hisa za makampuni yaliyoorodhesha hisa zake kwenye Soko la Hisa. Bodi iliamua kuwekeza kwenye maeneo yenye mapato ya uhakika (Amana za Serikali, Amana za Makampuni na faida inayotokana na Amana za Mabenki). Bodi ya Wakurugenzi inaamini kwa kuwekeza katika taasisi hizi za kifedha ni biashara nzuri kwa kuzingatia pale ambapo Soko la Hisa litashindwa kufanya vizuri kama ilivyo sasa ambapo kipato chake hakitabiriki.

Bodi ya Wakurugenzi imeamua kuelekeza uwekezaji wake kwenye amana za serikali kwa sababu faida yake ni ya uhakika ukilinganisha na uwekezaji katika hisa.

Mwisho, Bodi inapenda kuainisha maeneo mengine ya uwekezaji kama kuagiza na kuuza bidhaa nje ya nchi, wakala wa huduma ya bima, usindikaji wa mazao na maeneo mengine ya taasisi ya fedha kama ubadilishaji wa fedha za kigeni.

### MTAZAMO WA BODI

Bodi ya Wakurugenzi inatazamia taarifa ya Mahesabu inatoa picha kamili ya masuala ya kifedha ya Kampuni kama ilivyokuwa kufikia tarehe 31 Desemba, 2019 na faida/ hasara na mzunguko wa kifedha kwa mwaka kulingana na kanuni za uandaaji wa taarifa za mahesabu za Kimataifa na sheria ya makampuni ya mwaka 2002. Hata hivyo, hakuna chochote kinachoipa mashaka Bodi kwamba Kampuni itashindwa kuendelea na shughuli zake za biashara kwa miezi kumi na mbili (12) ijayo tangu kutolewa kwa hii taarifa ya mahesabu.

### WAKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI

Wakaguzi wa Mahesabu, Crowe Tanzania, wameendelea kuonyesha nia yao ya kuendelea kukagua mahesabu ya Kampuni endapo watateuliwa tena kukagua mahesabu ya Kampuni kwa mwaka wa fedha utakaoishia tarehe 31 Desemba, 2020. Hata hivyo, Bodi itawasilisha pendekezo la uteuzi wa mkaguzi katika dondoo zinazofuata.

Taarifa hii imeidhinishwa na Bodi katika Mkutano maalum uliofanyika tarehe 25/06/2020 na kusainiwa na wajumbe wafuatao:

.........................................

Fortunatus M. Magambo

Mkurugenzi

.........................................

Prof Lucian Msambichaka

Mkurugenzi

Tarehe : 25/06/2020

**Dondoo Na. 15/6/2020**

## WAJIBU WA WAKURUGENZI

Kulingana na sheria ya makampuni ya mwaka 2002, Bodi ina wajibu wa kuandaa taarifa ya mahesabu ya Kampuni na taarifa zingine zinazohusiana na hizo ambazo zimeunganishwa kwenye taarifa hii. Wakurugenzi wana jukumu la kuhakikisha kuwa taarifa ya fedha inatoa picha halisi ya Kampuni kila mwisho wa mwaka wa fedha na matokeo ya shughuli za Kampuni, mapato na matumizi ya fedha kwa kipindi ambacho kinamalizika, kulingana na Viwango vya Kimataifa vya uandaaji wa Taarifa za Fedha. Wakaguzi wa nje wanatakiwa kutoa maoni ya kujitegemea kwenye taarifa za fedha.

Wakurugenzi wana wajibu wa kusimamia na kudhibiti mfumo wa ndani wa kifedha uliowekwa na Kampuni na kuweka umuhimu mkubwa katika kudumisha mazingira mazuri ya udhibiti. Ili kuwawezesha wakurugenzi kufikia malengo haya, wanatakiwa kuweka mikakati ya kupunguza au kuondoa kabisa hasara kwa gharama yoyote. Hii inajumuisha mpangilio wa majukumu, na mgawanyo wa kazi. Wafanyakazi wote wanapaswa kudumisha kiwango cha juu cha maadili ili kuhakikisha kazi zinafanyika kwa usahihi na kuondoa mazingira yoyote yanayoweza kuisababishia Kampuni hasara.

Ni vizuri kutambua, kutathmini, kusimamia na kufuatilia aina zote za hatari katika kampuni. Athari katika uendeshaji wa shughuli za Kampuni haiwezi kuondolewa kabisa bali inaweza kupunguzwa kwa kuhakikisha kwamba miundombinu sahihi, udhibiti, mifumo na tabia ya kimaadili hutumiwa na kusimamiwa ndani ya taratibu zilizowekwa.

Maoni ya Wakurugenzi kutokana na maelezo waliyopokea kutoka kwa Menejimenti, ni kwamba mfumo wa udhibiti wa ndani unatoa uhakika kwamba, taarifa ya fedha zinaweza kutegemewa kwa ajili ya maandalizi ya taarifa ya mahesabu. Hata hivyo, mfumo wowote wa udhibiti wa kifedha wa ndani unaweza kutoa tu picha lakini sio uhakika dhidi ya kupotea au hasara iliyotokea.

Wakurugenzi wamepitia makisio ya utayarishaji wa Mahesabu ya Kampuni kwa mwaka huu unaoishia Desemba 31, 2019 na kwa mujibu wa tathmini hii na hali ya kifedha ya Kampuni kwa sasa, inaridhisha kuwa Kampuni ina rasilimali za kutosha na itaendelea kufanya vizuri.

Wakaguzi wa nje wanawajibika kukagua na kutoa taarifa ya mahesabu ya Kampuni. Taarifa ya mahesabu ya kampuni iliyokaguliwa imewasilishwa kwenye ukurasa wa 24 hadi 28 ambazo zimeandaliwa na kuidhinishwa na bodi ya Wakurugenzi na kusainiwa na:

| | |
|---|---|
| .................................. | .................................. |
| Fortunatus M. Magambo | Prof Lucian Msambichaka |
| Mkurugenzi | Mkurugenzi |

Tarehe : 25/06/2020

## MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 31/12/2019

## TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA 31/ 12/ 2019

| | 2019 | 2018 |
|---|---|---|
| | Sh '000 | Sh '000 |
| Mapato | 1,787,692 | 1,435,266 |
| Mapato mengine/ ( hasara) ya uendeshaji | (88,410) | (58,459) |
| Gharama nyingine za uendeshaji | (1,061,732) | (1,125,208) |
| **Faida ya uendeshaji** | **637,550** | **251,599** |
| Gharama za mtaji | (16,638) | – |
| **Faida/ ( hasara) kabla ya kodi** | **620,912** | **251,599** |
| Kodi | (211,198) | 170,792 |
| **Faida/ (hasara) kwa mwaka** | **409,714** | **422,391** |

| | | |
|---|---|---|
| Mapato mengine kamili | | |
| Kupanda/ (kushuka) kwa thamani ya hisa | (1,688,114) | (2,030,139) |
| **Mapato/ (hasara) mengine kwa mwaka** | (1,688,114) | (2,030,139) |
| **Jumla ya mapato/ (hasara) kwa mwaka** | **(1,278,400)** | **(1,607,748)** |
| **Mapato kwa kila hisa** | **5.62** | **5.78** |

## TAARIFA YA WARAKA WA MIZANIA HADI MWEZI WA KUMI NA MBILI 2019

| | 2019<br>Sh '000 | 2018<br>Sh'000 |
|---|---|---|
| **Rasilimali** | | |
| **Rasilimali za muda mrefu** | | |
| Mali ya kudumu inayogusika | 21,456 | 31,803 |
| Uwekezaji kwenye ardhi/majengo | 239,820 | 239,820 |
| Uwekezaji kwenye hisa | 19,364,888 | 22,988,002 |
| Dhamana za serikali | 9,677,922 | 4,249,239 |
| Kodi ilioahirishwa | 1,605 | 170,792 |
| Amana za makampuni/mashirika | 30,336 | 58,706 |
| Uwekezaji mwingine | 5,500 | 5,500 |
| | **29,341,527** | **27,743,862** |
| **Rasilimali za muda mfupi** | | |
| Rasilimali za biashara | 406,964 | 130,891 |
| Kodi ya muda mfupi | 340,051 | 331,318 |
| Fedha na thamani ya fedha | 224,314 | 650,849 |
| | 971,329 | 1,113,058 |
| **Jumla ya Rasilimali** | **30,312,856** | **28,856,920** |
| Mtaji na Madeni | | |
| Mtaji | 2,167,952 | 2,167,952 |
| Jumla ya akiba | 9,020,625 | (2,659,801) |
| Faida kuu | 15,907,804 | 28,866,632 |
| **Jumla** | **27,096,381** | **28,374,783** |

| | | |
|---|---|---|
| **Madeni ya muda mrefu** | | |
| Mkopo wa muda mrefu | 2,789,285 | - |
| Madeni ya muda mfupi | | |
| Madeni ya biashara | 44,289 | 20,364 |
| Mkopo wa muda mfupi | 210,715 | - |
| Gawio | 172,186 | 461,773 |
| | 427,190 | 482,137 |
| **Jumla ya madeni** | **3,216,475** | **482,137** |
| **Jumla ya mtaji na madeni** | **30,312,856** | **28,856,920** |

Taarifa hii ya mahesabu ilidhibitishwa kwa ajili ya kutangazwa na Bodi ya wakugurugenzi na zilisainiwa kwa niaba yao na:

Fortunatus .M.Magambo

Mwenyekiti

Tarehe 25/6/2020

Prof. Lucian A. Msambichaka

Mjumbe wa Bodi

Tarehe 25/6/2020

## TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI KWA MWAKA 2019

| | Mtaji wa Hisa | Mapato ya hisa | Jumla ya Mtaji wa Hisa | Akiba ya thamani ya uwekezaji kwenye hisa | Gharama ya IPO | Faida kuu | Jumla ya Mtaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mwaka uliopita | **Sh'000** | **Sh '000** | **Sh '000** | **Sh'000** | **Sh'000** | **Sh '000** | **Sh '000** |
| **Usawa tarehe 01/01/2018** | **1,459,153** | **708,799** | **2,167,952** | 2,726,439 | (629,662) | 28,629,939 | 32,894,666 |
| | | | | | | | |
| Faida ya mwaka | | | | | | 422,391 | 422,391 |
| Mapato mengine | | | | (4,756,578) | | | (4,756,578) |
| Gawio | | | | | | (185,698) | (185,698) |
| **Usawa tarehe 31/12/2018** | **1,459,153** | 708,799 | 2,167,952 | **(2,030,139)** | (629,662) | 28,866,632 | 28,374,781 |
| **Muda wa sasa:** | | | | | | | |
| **Usawa tarehe 01/01/2019** | **1,459,153** | 708,799 | 2,167,952 | **(2,030,139)** | (629,662) | 28,866,632 | 28,374,781 |
| Faida ya mwaka | | | | | | 409,714 | 409,714 |
| Mapato mengine | | | | 11,515,426 | | | 11,515,426 |
| Kuhamisha kwenda akiba kuu | | | | 165,000 | | (13,368,540) | (13,203,540) |
| **Usawa tarehe 31/12/2019** | 1,459,153 | 708,799 | 2,167,952 | 9,650,287 | (629,662) | 15,907,806 | 27,096,381 |

## TAARIFA YA MZUNGUKO WA FEDHA

| | 2019 Tsh '000 | 2018 Tsh '000 |
|---|---|---|
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uendeshaji** | | |
| Fedha iliyotoka kwenye shughuli za uendeshaji | 480,238 | 880,555 |
| Gharama za kifedha | (16,638) | - |
| Kodi iliolipwa | (50,743) | (70,535) |
| **Fedha taslimu inayotokana na uendeshaji** | **412,857** | **810,020** |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na uwekezaji** | | |
| Manunuzi ya mali ya kudumu inayogusika | (3,960) | (7,249) |
| Manunuzi ya mali ya kudumu inayogusika | 1,588 | - |
| Mauzo ya hisa za uwekezaji | 1,935,000 | 1,475,853 |
| Manunuzi ya dhamana za serikali | (5,428,683) | (4,249,239) |
| Mzunguko wa amana za kibenki | - | 2,272,580 |
| Kuiva kwa amana za mashirika | 28,370 | 28,369 |
| Faida/(hasara)inayotokana na kuuza hisa | (82,120) | (58,460) |
| **Fedha taslimu iliyotumika katika uwekezaji** | **(3,549,805)** | **(538,146)** |
| **Mzunguko wa fedha kutokana na mtaji** | | |
| Fedha kutoka kwenye mauzo ya hisa za kampuni | - | 746,104 |
| Feaha kutoka kwenye mkopo | 3,000,000 | - |
| Gawio | (289,587) | (19,652) |
| Gharama za kuuza husa za kampuni | - | (629,662) |
| **Fedha taslimu iliyotokana na mtaji** | **2,710,413** | **96,790** |
| **Jumla ya fedha taslimu za mzunguko kwa mwaka** | (426,535) | 368,664 |
| Fedha na thamani ya fedha mwanzo wa mwaka | 650,849 | 282,185 |
| **Fedha na thamani ya fedha mwisho wa mwaka** | **224,314** | **650,849** |

KUPOKEA, KUJADILI NA KURIDHIA TAARIFA YA WAKURUGENZI WA BODI YA KAMPUNI NA TAARIFA YA MAHESABU YALIYOKAGULIWA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 31 DESEMBA, 2019. TAARIFA YA FEDHA YA MWAKA ILIYOKAGULIWA IKO KATIKA TAARIFA YA MWAKA.

WASILISHO:

Ndugu Wanahisa mnaombwa kupokea na kuridhia Taarifa ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba, 2019 na kuaziamia kama ifuatavyo.

## “Azimio la 3/2020

**Taarifa ya Mwaka ya Wakurugenzi na Taarifa ya Fedha iliyokaguliwa kwa kipindi cha Mwaka ulioishia tarehe 31 Desemba 2019 imepitishwa kama ilivyowasilishwa.”**



**Dondoo Na. 15/7/2020**

## KUTANGAZA GAWIO

Kwa mwaka wa fedha ulioshia Desemba 2019 Bodi inapendekeza kulipa gawio la shilingi 6 kwa hisa (2018: shilingi 2.54 kwa hisa).

### Wasilisho

Bodi inapendekeza kuwa kama Mkutano Mkuu utaridhia pendekezo hili, malipo ya gawio kwa wanahisa yafanyike siku tisini (90) baada ya kupitisha azimio hili. Kwa wanahisa ambao wana akaunti za benki malipo yatalipwa kupitia kwenye akaunti zao na kwa njia ya mitandao ya simu.



> **"Azimio la 4/2020**
>
> **Mkutano Mkuu umeazimia, kuridhia pendekezo hili kwamba gawio la shilingi za Kitanzania Sita (6) kwa kila hisa kama ilivyopendekezwa na Bodi ya Wakurugenzi."**

**Dondoo Na. 15/8/2020**

## UTEUZI WA MKAGUZI WA MAHESABU YA KAMPUNI KWA MWAKA WA FEDHA UNAOISHIA DESEMBA 31, 2020

Kama ilivyoelezwa kwenye Taarifa ya Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Desemba 31, 2019, Mahesabu ya Kampuni yalikaguliwa na Kampuni ya Ukaguzi wa Mahesabu na Ushauri ya CROWE Tanzania. Hadi sasa Bodi imeridhika na kazi ambayo ilifanywa na Kampuni hii kwa mwaka 2019. Aidha Kampuni hiyo imeonyesha nia ya kuendelea kukagua Mahesabu ya Kampuni yetu kama watateuliwa tena.

### WASILISHO

Bodi inapendekeza kuwa CROWE Tanzania wateuliwe tena kukagua Mahesabu ya Kampani kwa mwaka unaoishia Desemba 31, 2020. Ada ya Ukaguzi inayopendekezwa ni kiasi cha Shilingi 19 milioni kabla ya VAT. Ada inayopendekezwa na Bodi imezingatia mwenendo wa Soko kwa taaluma ya Uhasibu na Ukaguzi, ukuaji wa shughuli za Kampuni na mfumuko wa bei nchini.

## “Azimio la 5/2020

**Imeazimiwa kukubaliana na pendekezo la Bodi ya Wakurugenzi kuwa CROWE Tanzania waendelee kukagua Mahesabu ya Kampuni kwa Mwaka wa Fedha unaoishia Desemba 31, 2020. Pamoja na kuidhinisha Shilingi 19 milioni kama gharama za malipo ya ukaguzi wa mehesabu ya Kampuni.”**



**Dondoo Na.15/9/2020**

## PENDEKEZO KUHUSU MALIPO YA WAKURUGENZI

Malipo ya Wajumbe wa Bodi, [Directors fees] yameainishwa kwenye Katiba ya Kampuni. Kifungu Namba 70 [i] kinaeleza kuwa: "The remuneration of the Directors shall from time to time be determined by the Company in General Meeting".

Malipo haya huwa yanawekwa kwenye Bajeti ya Kampuni kila mwaka. Malipo ya Wajumbe yanatokana na ukweli kuwa Wajumbe wa Bodi hutumia muda mwingi kusimamia shughuli za Kampuni, badala ya kusimamia shughuli zao binafsi. Ikumbukwe kuwa Wajumbe wa Bodi ndio wanawajibika kwa Mkutano Mkuu kwa kusimamia shughuli za Kampuni kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Makampuni ya Mwaka 2002, pamoja na kanuni na taratibu zilizowekwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Hisa la Dar-es-Salaam, utawala bora na ufanisi wa Kampuni. Kwa kifupi chini ya Sheria ya Makampuni, Wajumbe wanawajibika kuhakikisha kuwa wanasimamia vema Kampuni ili wanahisa wasipoteze fedha zao na kwamba mtaji wa Kampuni unakua.

### WASILISHO

Kwa kuzingatia matokeo ya shughuli za Kampuni kwa Mwaka wa fedha ulioishia Desemba 31, 2019, Menejimenti inapendekeza kuwa Wajumbe wa Bodi walipwe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000), kiasi hichi kimezingatia mazingira ya sasa na pia Wakurugenzi walikuwa wakilipwa kiasi cha shilingi milioni nne kwa kwa kipindi cha miaka minne.



**"Azimio la 6/2020**

**Imeazimiwa kwamba kama ilivyopendekezwa na Menejimenti, malipo ya Wakurugenzi wa Bodi yawe Shilingi milioni nne na laki nane (Shilingi 4,800,000) kwa kila Mjumbe wa Bodi."**

| | ORODHA YA WALIOHUDHURIA | KIAMBATISHO 1 | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Hisa Na. | Jina la Mwanahisa | Hisa | % | Aina |
| 1 | 51121 | PUBLIC SERVICE SOCIAL SECURITY FUND | 28,100,300 | 38.45 | Mwanahisa |
| 2 | 569364 | MKOMBOZI FISHING & MARING TRANSPORT LTD | 4,215,000 | 5.77 | Mwanahisa |
| 3 | 150344 | CHRISTOPHER MWITA GACHUMA | 1,405,000 | 1.92 | Mwanahisa |
| 4 | 121481 | FAYAZ FEROZ RASHID | 1,236,400 | 1.69 | Mwanahisa |
| 5 | 149308 | ELVIS ARISTABLUS MUSIBA | 674,375 | 0.92 | Mwanahisa |
| 6 | 105271 | LUCIAN AMBROSE MSAMBICHAKA | 464,200 | 0.64 | Mwanahisa |
| 7 | 569170 | JANE ROBERT MASABARI | 281,000 | 0.38 | Mwanahisa |
| 8 | 569210 | ALOIS JOSEPH MWAMANGA | 231,975 | 0.32 | Mwanahisa |
| 9 | 569202 | DR. STERGOMENA LAWRENCE TAX | 168,600 | 0.23 | Mwanahisa |
| 10 | 83945 | FRANK TIMOTH MSUYA | 168,575 | 0.23 | Mwanahisa |
| 11 | 569265 | DR. GIDEON HOSEA KAUNDA | 112,400 | 0.15 | Mwanahisa |
| 12 | 569352 | CROWN TECH - CONSULT LTD | 112,400 | 0.15 | Mwanahisa |
| 13 | 569147 | HAMAD JUMBE MENYE | 84,800 | 0.12 | Mwanahisa |
| 14 | 569696 | COSMAS MORIS HONERA | 70,250 | 0.10 | Mwanahisa |
| 15 | 569907 | MOHAMED BURHAN | 56,200 | 0.08 | Mwanahisa |
| 16 | 569279 | DR. VICENT ISAAC MHADA | 56,200 | 0.08 | Mwanahisa |
| 17 | 569325 | TCCIA DAR ES SALAAM | 56,200 | 0.08 | Mwanahisa |
| 18 | 569448 | JANETH ELIHUDI MDINGI | 56,200 | 0.08 | Mwanahisa |
| 19 | 107183 | MOHAMEDRAFIK AKBER PARPIA | 56,200 | 0.08 | Mwanahisa |
| 20 | 127797 | WILFRED MUTASHOBYA KAMUNTU | 56,200 | 0.08 | Mwanahisa |
| 21 | 128185 | FRUMENCE JOACHIM SHIRIMA | 56,200 | 0.08 | Mwanahisa |
| 22 | 569102 | ADOLPH MICHAEL SHOKI | 49,150 | 0.07 | Mwanahisa |
| 23 | 569326 | TCCIA DODOMA | 44,962 | 0.06 | Mwanahisa |
| 24 | 165515 | EVELINE AMASIA MWETA | 42,150 | 0.06 | Mwanahisa |
| 25 | 98946 | SALEEM AKBER PARPIA | 30,900 | 0.04 | Mwanahisa |
| 26 | 569332 | TCCIA MBEYA | 28,100 | 0.04 | Mwanahisa |
| 27 | 569334 | TCCIA MTWARA | 28,100 | 0.04 | Mwanahisa |
| 28 | 569337 | TCCIA SHINYANGA | 28,100 | 0.04 | Mwanahisa |
| 29 | 569976 | NGOMUO INVESTIMENT | 22,475 | 0.03 | Mwanahisa |
| 30 | 569799 | BRUNO JUMA NGUMUO | 16,863 | 0.02 | Mwanahisa |
| 31 | 70522 | ELIFASI ELINIMO MSWIA | 16,863 | 0.02 | Mwanahisa |
| 32 | 569184 | JOEL TIMOTH CHIKOMA | 14,613 | 0.02 | Mwanahisa |
| 33 | 569341 | TCCIA COAST | 14,050 | 0.02 | Mwanahisa |
| 34 | 569336 | TCCIA RUKWA | 14,050 | 0.02 | Mwanahisa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 35 | 569331 | TCCIA LINDI | 14,050 | 0.02 | Mwanahisa |
| 36 | 546726 | JOSEPH MATANGA KAHUNGWA | 12,500 | 0.02 | Mwanahisa |
| 37 | 228299 | ISARIA KAWEDI MWENDE | 12,500 | 0.02 | Mwanahisa |
| 38 | 514523 | DONALD JIMOGI KAMORI | 12,500 | 0.02 | Mwanahisa |
| 39 | 219736 | DONALD JIMOGI KAMORI | 11,238 | 0.02 | Mwanahisa |
| 40 | 123540 | JOSEPH ANAELI NDOSSA OMBAELI | 10,000 | 0.01 | Mwanahisa |
| 41 | 569168 | KENNEDY NELSON SIMUNDI | 9,985 | 0.01 | Mwanahisa |
| 42 | 569578 | GODFREY MDACHI HIZA | 8,425 | 0.01 | Mwanahisa |
| 43 | 165035 | CHARLES PARADISO URASA | 6,250 | 0.01 | Mwanahisa |
| 44 | 46261 | CHARLES AWEDA GORANGA | 5,625 | 0.01 | Mwanahisa |
| 45 | 569329 | TCCIA KIGOMA | 5,625 | 0.01 | Mwanahisa |
| 46 | 88062 | SYNPHOROSE EVARIST BAITWA | 5,000 | 0.01 | Mwanahisa |
| 47 | 120764 | JEHOVA ROMWALD MGONJA | 5,000 | 0.01 | Mwanahisa |
| 48 | 514977 | MBAZI ISAAC MDINGI | 5,000 | 0.01 | Mwanahisa |
| 49 | 569197 | EDGAR JOEL KAHABWA | 4,413 | 0.01 | Mwanahisa |
| 50 | 569522 | NAANJELA PAUL MSANGI | 4,212 | 0.01 | Mwanahisa |
| 51 | 569430 | ALFRED SALUM NDEGIPARA | 3,375 | 0.00 | Mwanahisa |
| 52 | 569633 | SAMWEL SYLVESTA LAYDER | 2,812 | 0.00 | Mwanahisa |
| 53 | 52430 | MAGDALENE NELSON ENOCK MKOCHA | 102,263 | 0.00 | Mwanahisa |
| 54 | 569330 | TCCIA - KILOMBERO | 1,400 | 0.00 | Mwanahisa |
| 55 | 569698 | DONALD NZAGA WARIOBA | 1,400 | 0.00 | Mwanahisa |
| 56 | 570779 | ABSALOM NDELILID NNKO | 1,400 | 0.00 | Mwanahisa |
| 57 | 570880 | GUERNOUS COSMAS MGINA | 1,400 | 0.00 | Mwanahisa |
| 58 | 546691 | COLETHA CHARLES PARADISO | 1,250 | 0.00 | Mwanahisa |
| 59 | 546276 | EMMANUEL EUSTACE ISHASI | 400 | 0.00 | Mwanahisa |
| 60 | 546793 | DONALD NZAGA WARIOBA | 150 | 0.00 | Mwanahisa |
| 61 | 546365 | DORICA ELIA NYANGUSI | 100 | 0.00 | Mwanahisa |
| 62 | 546505 | GEOFFREY ROBERT NYANGUSI | 100 | 0.00 | Mwanahisa |
| 63 | 546275 | EMMANUEL E. ISHASI | 100 | 0.00 | Mwanahisa |
| 64 | 510671 | RONALD KATO | 100 | 0.00 | Mwanahisa |
| 65 | 232527 | JAIROS YAHYA FWIMI | 40 | 0.00 | Mwanahisa |
| | | | **38,217,201** | **52** | |

**TCCIA INVESTMENT PLC**
LAPF Millenium Tower 2, 24th Floor,
Opposite Makumbusho Village
P. O. Box 72678 Dar es Salaam, Tanzania
Tel: 255 – 22 – 276 0172/27601725
Fax: 255 – 22 – 2119437
Email: info@tcciainvest.co.tz,
Web site: http://www.tcciainvest.co.tz